



## Chanjo

Ili upate malipo ya familia kwa mtoto chini ya umri wa miaka 20, unahitaji kuhakikisha amepata chanjo zote kwa umri wake.

### Ni malipo gani yanayoathirika?

- Faida ya Kulea Watoto (Child Care Benefit)
- Kipunguzo cha Kulea Watoto (Child Care Rebate), na
- Nyongeza ya Sehemu A ya Faida ya Ushuru wa Familia (Family Tax Benefit Part A supplement)

Mabadiliko haya yatawaathiri pia wateja wanaodai, Faida ya Babu/Bibi Kulea Watoto (Grandparent Child Care Benefit), Faida Maalum ya Kulea Watoto (Special Child Care Benefit) au Usaidizi wa Ada ya Kuwalea Watoto wakati wa Kazi, Elimu na Mafunzo (Jobs, Education and Training Child Care Fee Assistance).

### Kwa nini upate chanjo?

Chanjo hukuweka wewe na watoto wako mkiwa wenye afya na salama dhidi ya magonjwa mabaya. Ni rahisi, salama na inafanya kazi.

### Ninahitaji kufanya nini?

Ili utimize mahitaji ya chanjo, mtoto wako anahitaji:

- kuwa amepata chanjo zake zote za utotoni, au
- ana sababu ya kimatibabu ya kutochanjwa.

Tutakagua maelezo ya chanjo ya mtoto wako kwenye Sajili ya Chanjo ya Australia (Australian Immunisation Register) kwa kutumia maelezo yake ya Medicare.

Watoto ambao hawastahili kujiandikisha katika Medicare wataongezwa kwenye Sajili ya Chanjo ya Australia (Australian Immunisation Register) wakati mtoa huduma ya chanjo (pamoja na daktari) anapotuma maelezo ya chanjo kwa Sajili ya Chanjo ya Australia (Australian Immunisation Register).

Ongea na daktari wako ikiwa kuna sababu ya kimatibabu ambayo inamfanya mtoto wako asiweze kupata chanjo.

## Nitajuaje kama mtoto wangu amepata chanjo zake zote za umri wake?

Unaweza kukagua taarifa ya historia ya chanjo ya mtoto wako kwa kutumia:

- akaunti yako ya mtandaoni ya Medicare kupitia myGov. Ikiwa huna akaunti ya myGov, fungua moja na uiunganishe kwenye akaunti yako ya mtandaoni ya Medicare
- programu ya vifaa vya mkononi ya Express Plus Medicare. Ikiwa huna programu hii, ipakue kwenye App Store, Google Play™ na vifaa kadhaa vya mkononi na kompyuta zinazotumia Windows 10.

Watu walio na umri wa miaka 14 au zaidi wanaweza kupata taarifa yao ya historia ya chanjo:

- kwa kutumia akaunti yao wenyewe ya mtandaoni ya Medicare kupitia myGov
- kwa kutumia programu ya vifaa vya mkononi ya Express Plus Medicare au
- kupiga simu **1800 653 809**.

Ikiwa kuna maelezo yanayokosekana kutoka kwa taarifa ya historia ya chanjo ya mtoto wako, muulize mtoa huduma wako wa chanjo ayatume kwa Sajili ya Chanjo ya Australia (Australian Immunisation Register).

## Chanjo ya nje ya nchi

Ikiwa mtoto wako alipokea chanjo nje ya nchi, peleka dhibitisho za chanjo hizi kwa mtoa huduma wako wa chanjo wa Australia. Atakagua mtoto wako kama amepata chanjo sahihi zinazotimiza Ratiba ya Mpango wa Kitaifa wa Chanjo nchini Australia (Australian National Immunisation Program).

Ikiwa mtoto wako ametimiza Ratiba ya (National Immunisation Program Schedule), mtoa huduma wako wa chanjo wa Australia atasasisha Sajili ya Chanjo ya Australia (Australian Immunisation Register).

Ikiwa mtoto wako hatimizi Ratiba ya (National Immunisation Program Schedule), mtoa huduma huyo wa chanjo atapendekeza ratiba ya kupata chanjo hizi.

Ikiwa umewasili hivi karibuni nchini Australia na unahitaji ushahidi wa chanjo za mtoto wako utafsiriwe, soma zaidi kuhusu [Huduma za Tafsiri Bila Malipo \(Free Translating Service\)](#) kwenye tovuti ya Idara ya Huduma za Jamii (Department of Social Services).

## Sajili ya Chanjo ya Australia (Australian Immunisation Register)

Sajili ya Chanjo ya Australia (Australian Immunisation Register) ni sajili ya kitaifa ambayo hurekodi chanjo zilizopewa watu wa umri wote nchini Australia. Sajili hii hurekodi chanjo zinazotolewa na madaktari na kliniki za jumuia.

Tutawajumuisha moja kwa moja watoto walioandikishwa katika Medicare kwenye Sajili ya Chanjo ya Australia (Australian Immunisation Register).

Tutawaongeza watoto ambao hawastahili kujiandikisha katika Medicare kwenye Sajili ya Chanjo (Immunisation Register) wakati mtoa huduma ya chanjo (pamoja na daktari) anapotuma maelezo ya chanjo kwa Sajili ya Chanjo ya Australia (Australian Immunisation Register).

## Kwa maelezo zaidi

- nenda kwenye [humanservices.gov.au/air](https://humanservices.gov.au/air) kwa maelezo zaidi ya Kiingereza.
- nenda kwenye [humanservices.gov.au/yourlanguage](https://humanservices.gov.au/yourlanguage) ambapo unaweza kusikiliza au kutazama video zenye maelezo kwa Kiswahili
- piga simu **131 202** ili uongee na sisi kwa Kiswahili kuhusu malipo na huduma za Centrelink
- pigia simu Huduma ya Tafsiri na Ukalimani (Translating and Interpreting Service (TIS National)) kwa nambari ya simu **131 450** ili uongee na sisi kwa Kiswahili kuhusu Medicare na malipo na huduma za Kuwalea Watoto (Child Support)
- tembelea kituo cha huduma.

Kumbuka: simu kutoka kwa simu yako ya nyumbani kwa nambari '13' kutoka mahali popote Australia hulipishwa ada moja. Kiwango hicho kinaweza kutofautiana na bei ya simu za nchini na kinaweza pia kutofautiana kati ya watoa huduma ya simu. Simu kwa nambari '1800' kutoka kwa simu yako ya nyumbani hazina malipo. Simu kutoka kwa simu za umma au za mkononi zinaweza kuwekewa muda na kulipishwa kiwango cha juu.

## Kanusho

Maelezo yaliyo katika chapisho hili yamekusudiwa kama mwongozo wa malipo na huduma. Ni wajibu wako kuamua kama unataka kuomba malipo na kutuma maombi yanayohusiana na hali zako maalum.



# Immunisation

To get a family payment for a child under 20 years of age, you need to make sure their immunisations are up to date.

## What payments are affected?

- Child Care Benefit
- Child Care Rebate, and
- Family Tax Benefit Part A supplement

These changes will also affect customers who claim Grandparent Child Care Benefit, Special Child Care Benefit or Jobs, Education and Training Child Care Fee Assistance.

## Why immunise?

Immunisation keeps you and your children healthy and safe from harmful diseases. It's simple, safe and effective.

## What do I need to do?

To meet the immunisation requirements, your child needs to:

- be up to date with their early childhood immunisations, or
- have a medical exemption.

We'll check your child's immunisation details on the Australian Immunisation Register using their Medicare details.

Children who aren't eligible to enrol in Medicare will be added to the Immunisation Register when a vaccination provider (including a general practitioner) sends the details of a vaccination to the Australian Immunisation Register.

Talk to your general practitioner if there's a medical reason why your child can't be vaccinated.

## How do I know if my child is up to date with their immunisations?

You can check your child's immunisation history statement using:

- your Medicare online account through myGov. If you don't have a myGov account, create one and link it to your Medicare online account
- the Express Plus Medicare mobile app. If you don't have the app, download it from the App Store, Google Play™ and selected Windows 10 mobile devices and desktops.

Individuals 14 years of age or older can access their immunisation history statement:

- using or creating their own Medicare online account through myGov
- using the Express Plus Medicare mobile app or
- calling **1800 653 809**.

If there's information missing from your child's immunisation history statement, ask your vaccination provider to send it to the Australian Immunisation Register.

## Overseas vaccinations

If your child received vaccinations overseas, take proof of these to your Australian vaccination provider. They'll check your child has been given the correct vaccinations to meet the Australian National Immunisation Program Schedule.

If your child has met the National Immunisation Program Schedule, your Australian vaccination provider will update the Australian Immunisation Register.

If your child doesn't meet the National Immunisation Program Schedule, the vaccination provider will recommend a catch up schedule of vaccinations.

If you've recently arrived in Australia and need your child's immunisation evidence translated, read more about the [Free Translating Service](#) on the Department of Social Services website.

## Australian Immunisation Register

The Australian Immunisation Register is a national register that records vaccinations given to people of all ages in Australia. The register records vaccinations given through general practices and community clinics.

We will automatically include children enrolled in Medicare on the Australian Immunisation Register.

We will add children who aren't eligible to enrol in Medicare to the Immunisation Register when a vaccination provider (including a general practitioner) sends the details of a vaccination to the Australian Immunisation Register.

## For more information

- go to [humanservices.gov.au/air](https://humanservices.gov.au/air) for more information in English
- go to [humanservices.gov.au/yourlanguage](https://humanservices.gov.au/yourlanguage) where you can read, listen to or watch videos with information in your language
- call **131 202** to speak with us in your language about Centrelink payments and services
- call the Translating and Interpreting Service (TIS National) on **131 450** to speak with us in your language about Medicare and Child Support payments and services
- visit a service centre.

Note: calls from your home phone to '13' numbers from anywhere in Australia are charged at a fixed rate. That rate may vary from the price of a local call and may also vary between telephone service providers. Calls to '1800' numbers from your home phone are free. Calls from public and mobile phones may be timed and charged at a higher rate.

## **Disclaimer**

The information contained in this publication is intended only as a guide to payments and services. It's your responsibility to decide if you wish to apply for a payment and to make an application with regard to your particular circumstances.